


# Eastern Africa Journal of Kiswahili

[ISSN 2958-1036]
**Volume: 05 Issue: 01 | September-2026**

EAJK


# Athari Za Lugha Ya Kijinsia Katika Kusuluhisha Changamoto Za Kiekolojia Katika Riwaya Ya Nakuruto (2009) Ya Clara Momanyi


**Authors**

**Okebe Bildad Okoth [(1)]; Odoyo Benard Okal [(2)]; Owen Mconyango [(3)]**

**Main author's email: okebe.bildad@gmail.com**

**(1.2.3) Maseno University Kenya.**



**Cite this article in APA**

Okoth, O. B., Okal, O. B., & Mconyango, O. (2026). Athari za lugha ya kijinsia katika kusuluhisha changamoto za kiekolojia katika riwaya ya Nakuruto (2009) ya Clara Momanyi. *Eastern Africa journal of Kiswahili*, 5(1), 144-152. https://doi.org/10.51317/eajk.v5i1.1175

OPEN ACCESS A publication of Editon Consortium Publishing (online)

**Article history**
Received: 2026-07-12
Accepted: 2026-08-15
Published: 2026-09-10


**Scan this QR to read the paper online**


**Copyright**: ©2026 by the author(s). This article is an Open Access article distributed under the terms and conditions of the Creative Commons Attribution-NonCommercial-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-NC-SA 4.0).



**Ikisiri**

Makala hii ililenga kutathimini athari za lugha ya kijinsia katika kusuluhisha changamoto za kiekolojia katika riwaya ya *Nakuruto* (2009) ya Clara Momanyi. Mabadiliko ya ekolojia yameathiri binadamu kutokana na matukio makali ya hali ya anga yanayoletwa na mabadiliko ya tabianchi. Mabadiliko haya yamkini yanaonekana kuwa na athari tofauti kwa namna jinsia hizi zinavyokabiliana na kutekeleza majukumu yao. Ingawa taaluma nyingi zinaendelea kutafuta suluhisho la athari za mabadiliko ya ekolojia, ni wazi kuwa suluhisho kamili halijapatikana. Fasihi haijabaki nyuma katika utoaji wa mchango wake kuhusu ekolojia. Hata hivyo, tafiti chache tu ndizo zimejaribu kuhusisha fasihi ekolojia huku zikilenga mtazamo wa mwandishi au jinsia ya kike katika uhakiki wa makala mbalimbali za fasihi. Kwa hivyo, kuna haja ya kuangazia jinsia zote za kike na kiume katika utafutaji wa suluhisho kuhusu mabadiliko ya tabianchi. Utafiti huu ulielekezwa na lengo mahususi ya kutathmini athari za lugha ya kijinsia katika kusuluhisha changamoto za kiekolojia katika riwaya ya *Nakuruto*. Utafiti uliongozwa na Nadharia ya Ekofeministi. Muundo elezi ulitumika katika utafiti huu. Data zilichangunuliwa kulingana na lengo la utafiti na kuwasilishwa kimaelezo. Aidha usampulishaji dhamirifu wa kivigezo ulitumika kupata za kimsingi na za sekondari. Orodhahakiki na dodoso zilitumika kama vifaa. Utafiti ulibaini kuwa jinsia zote zina nafasi sawa katika kuleta suluhisho kwa changamoto za kiekolojia. Utafiti huu ulibainisha kuwa taaluma ya fasihi ina jukumu la kuwasilisha suluhisho kwa changamoto zinazosababishwa na mabadiliko ya ekolojia. Pia ulichangia mijadala ya uhakiki wa matumizi ya lugha kijinsia kuhusu maswala ya ekolojia



**Maneno muhimu:** Ekolojia, fasihi, jinsia, lugha, mabadiliko.

**UTANGULIZI**

Makala hii iliangazia athari za lugha ya kijinsia katika kusuluhisha changamoto za kiekolojia katika Riwaya teule ya *Nakuruto* (Momanyi, 2009). Kwa mujibu wa kongamano la bara la Afrika lililofanyika Nairobi, nchini Kenya linalofahamika kama Tamko la Nairobi na viongozi wa bara la Afrika (2023), kuhusu mabadiliko ya hali ya anga, ilibainika kwamba bara la Afrika linaathiriwa zaidi na mabadiliko katika hali ya hewa na ambapo jamii ya kimataifa ilitakiwa kuchukua hatua ya mapema na haraka kusaidia bara la Afrika kupambana na mabadiliko ya tabianchi. Mabadiliko haya, huathiri wananchi na nchi nzima kwa namna mbalimbali ikiwemo ukosefu wa lishe bora, kuzoreteka kwa uchumi, kudhoofika kwa amani na usalama wa nchi. Aidha, kongamano hili liliweka bayana kuwa changamoto zinazosababishwa na mabadiliko katika hali ya anga, zimesababishwa na matendo hasi ya binadamu. Hivyo basi, kila mmoja katika jamii ya kiafrika anahitajika kujihusisha katika utunzi wa vipengele mbalimbali vya ekolojia.

Kulingana na taarifa ya British Broadcasting Corporation (BBC) kuhusu sayansi na hali ya anga, Rannard na Stallard (2022) wanaweka bayana kwamba mabadiliko ya hali ya anga na ekolojia ni changamoto zinazoendelea kuwapa binadamu wasiwasi duniani kote, huku jinsia mbalimbali zikipata athari kwa viwango tofauti. Wanawake, makundi ya watu waliotengwa, watu wenye kipato cha chini na watoto hupata athari kubwa zaidi kutokana na mabadiliko haya. Viongozi wa nchi za madola na nchi nyinginezo wamejaribu kutafuta tiba la janga hili ila hawajapata suluhisho la kudumu. Katika mkutano wa Umoja wa Mataifa, uliofanyika Paris mwaka wa 2021, kuangazia maswala ya mabadiliko ya hali ya anga, katibu mkuu Bw. Ban Ki-Moon, alieleza kuwa kila bara linapata athari kali ya mabadiliko ya hali anga. Hali ambapo tayari imekuwa tishio kwa maendeleo ya kiuchumi na amani ya kimataifa. Katika mkutano huo, zaidi ya viongozi wa nchi za madola wapitao mia moja hamsini walihudhuria, kila mmoja akielezea viwango tofauti tofauti vya athari za mabadiliko ya hali ya anga kutoka nchi zao huku wote wakitafuta usaidizi wa kila namna ya kulegeza makali yanayosababishwa na athari hizo za majanga ya kimazingira.

Kulingana na ripoti ya Intergovernmental Panel on Climate Change (IPCC, 2014), iliyohusisha michango ya Makundi ya Kazi I, II na III, ongezeko la joto duniani katika miongo ya hivi karibuni limehusishwa kwa kiasi kikubwa na shughuli za binadamu, hususan uzalishaji wa gesi chafuzi. Mabadiliko haya ya tabianchi yameendelea kuathiri mifumo ya ekolojia na maisha ya binadamu duniani kote. Majanga haya ya kimazingira hukumba kila mmoja katika jamii bila kubagua maeneo yao ya makazi, na maamuzi na mitazamo yetu kuhusiana na uharibifu wa mazingira ndiyo hukinzana na kutofautiana.

Mbali na hayo, ekolojia yetu imo katika hali ya hatari ya maangamizi kutokana na matendo ya kibinafsi ya wanadamu. Matendo kama vile ukataji miti, ongezeko la teknolojia haribifu na ukosefu wa uongozi adilifu ambayo husababisha ongezeko la joto hewa na kuvugutwa kwa sayari, magonjwa, vifo na kupungua kwa mazao ni hali inayosababisha ongezeko kwa makali ya njaa.

Hivyo basi, taaluma nyingi za kisayansi, kiteknolojia na kimazingira zimejitokeza kutoa michango kuhusu utatuzi wa hali ya anga na ekolojia. Mbali na taaluma hizi, fasihi vilevile haijabaki nyuma katika utoaji wa mchango wake. Hata hivyo, tafiti chache ndizo zimeshughulikia maswala ya fasihi ekolojia licha ya kuwa huu ni uwanja mpya katika taaluma ya fasihi. Tafiti hizi chache zimelenga mtazamo wa mwandishi na pia nafasi ya jinsia ya kike pekee katika mijadala ya masuala ya ekolojia. Hali hii hutokea licha ya kuwa kimsingi fasihi ni kioo cha jamii na hivyo basi ina majukumu ya kuwasilisha hali kamili ya maisha ya mwanadamu kama vile ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na hali ya mazingira inayojumuisha anga na ekolojia, kwani matukio mengi katika jamii yana uhusiano mkubwa na fasihi (Matti, 2003)

**Dhana ya Fasihi Ekolojia**

Waandishi mbalimbali wamejitokeza kuzungumzia swala la fasihi ekolojia. Hata hivyo, kila mwandishi ana mtazamo wake kuhusu swala la ekolojia na namna anuai ya kulikabili. Waandishi kama vile Momanyi (2009) amezungumzia masuala ya mazingira katika riwaya ya *Nakuruto*. Riwaya ya *Nakuruto* inazungumzia vipengele mbalimbali vya ekolojia na changamoto tofauti tofauti zinazoleta majanga ya kimazingira kwa vipengele hivyo. Wamitila (2003) naye akawasilisha maudhui ya mazingira katika riwaya zake mbili za *Msimu wa Vipepeo* na *Tikiti Maji*. Aidha, alibainisha

vyanzo vya changamoto zinazosababisha majanga ya kimazingira na vilevile alipendekeza suluhisho faafu kwa matatizo hayo ya kimazingira. Mberia (2001) akazungumzia swala la mazingira katika mkusanyiko wa mashairi hasa Bara Jingine; naye Mbogo (2002) ameandikia swala la fasihi ekolojia katika riwaya ya *Bustani ya Edeni*.

Odum (1971) anasema kuwa ekolojia ni taaluma ya kisayansi inayochunguza mfumo na umuhimu wa maumbile ya kiasilia. Umuhimu wa mfumo wa ekolojia mara nyingi huathiriwa na namna jinsia mbalimbali zinavyohusiana na mazingira yao. Maoni haya yanaendelezwa na Krebs (1978) anapofafanua ekolojia kama taaluma ya kisayansi inayohusisha uchunguzi wa mtagusano na uhusiano kati ya jinsia moja na nyingine, wanyama mbalimbali na hata mimea. Maelezo haya yanathibitisha kuwa ekolojia ni taaluma ambayo inachunguza uhusiano na mtagusano baina ya waja na mazingira wanamoishi. Mazingira haya yanaweza kuwa msitu, mto, bahari, hali ya anga na hata mabadiliko ya hali ya anga. Isitoshe, mazingira haya yanaweza yakajumuisha maswala ya uchumi, siasa utamaduni na familia. Kwa upande mwingine, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (2019) inarejelea ekolojia kama tawi la biolojia linaloshughulikia uhusiano baina ya viumbehai na mimea na mazingira wanamoishi. Japo ekolojia ni swala la biolojia, taaluma ya fasihi vilevie inaienzi katika chambuzi za kazi anuai kama tunavyoona katika ekolojia ya fasihi.

Kulingana na Libre (2022), ekolojia ni uchunguzi unaohusu mwingiliano wa viumbe vilivyo hai na mazingira yao husika. Wanaekolojia huuliza maswali katika ngazi nne za shirika la kibiolojia-viumbe, jamii, idadi ya watu na mazingira. Katika ngazi ya viumbe, wanaekolojia hujifunza viumbe binafsi na jinsi wanavyoingiliana na mazingira yao. Katika viwango vya idadi ya watu na jamii, wanaekolojia wanachunguza jinsi idadi ya viumbe hai inavyobadilika baada ya kipindi fulani na njia ambazo idadi hiyo ya watu huingiliana na viumbe wengine katika jamii. Wanaekolojia wanaojifunza maswala ya mazingira, huchunguza vipengele hai vya mazingira kama vile misitu, wanyama mifugo na wa pori, binadamu, na vile visizohai katika mazingira kama vile maji, udongo, hewa.

Mabadiliko ya kiekolojia yameendelea kuathiri binadamu kutokana na matukio makali ya hali ya anga yanayosababishwa na mabadiliko ya tabianchi huku jinsia ya kike na ya kiume zikitafuta namna ya kukabiliana na hali hii. Mabadiliko haya husababishwa hususan na matendo ya binadamu ambayo huathiri vipengele mbalimbali vya ekolojia. Vipengele hivi vinapoathirika, basi huzua changamoto zinazohitaji kusuluhishwa upesi kitaaluma. Kutokana na tofauti kubwa iliyomo katika majukumu ya kijamii kwa kuangazia jinsia ya kike na kiume, mabadiliko ya ekolojia vilevile yanaonekana kuwa na athari tofauti kwa namna jinsia hizi zinavyokabiliana na kutekeleza majukumu yao kijamii na kiuchumi.

**Misingi ya Kinadharia**

Utafiti uliongozwa na Nadharia ya Ekofeministi. Kwa mujibu wa Glotfelty et al. (1996) Ekofeministi ni tawi la ufeministi linalozingatia usawa wa kijinsia, uhusiano kati ya mazingira na wanawake na makundi yaliyotengwa kama swala la kimsingi katika shughuli zake. Nadharia ya Ekofeministi iliasisiwa na Mfaransa Francoise d`bonne katika karne ya ishirini na ikaendelezwa na Glotfelty, Fromm na Buell katika miaka ya 1996, walipokuwa wakizindua kwa mara nyingine uwanja wa fasihi ekolojia iwe mojawapo la somo katika fasihi ulimwenguni. Nadharia ya Ekofeministi imekua na kupata nguvu mpya tangu ilipoanza katikati ya karne ya kumi na nane. Uhamasishaji kuhusu mabadiliko ya hali ya anga ulipoanza na kuendelea katika karne ya hivi karibuni, ndivyo ufeministi ulivyoanza kubainisha njia ambazo uhamasishaji kuhusu usawa wa kijinsia unavyoingiliana na uhifadhi na ukuzaji wa mazingira.

Dhana ya Ekofeministi iliendelezwa katika kazi ya Françoise d'Eaubonne ya *Le Féminisme ou la Mort* (1974). Kulingana na mtazamo wa Ekofeministi, dhuluma na ukosefu wa usawa wa kijinsia, pamoja na unyonyaji wa makundi yaliyotengwa katika jamii, vinaweza kuhusishwa na uharibifu wa mazingira kupitia mifumo ya mamlaka na utawala. Stoddart na Tindall (2011) wanaeleza uhusiano kati ya ufeministi na siasa za mazingira na kuonyesha namna dhana ya mfumo dume inavyotumika kuelewa uhusiano kati ya jinsia na mazingira. Aidha, wanaonyesha kuwa dhana ya *hegemonic masculinity* imekuwa muhimu katika kueleza namna wanawake na mazingira wanavyoweza kuathiriwa na mifumo tawala ya kiuchumi na kisiasa.

Kwa mtazamo wa Ekofeministi, hivyo, masuala ya mazingira, usawa wa kijinsia na miundo ya kijamii yanapaswa kuchunguzwa kwa pamoja (Stoddart & Tindall, 2011).

**Mihimili ya Ekofeministi**

Nadharia ya Ekofeministi inaongozwa na kanuni mbalimbali. Kanuni hizi ni kama zifuatazo: Kwanza, kwa mujibu wa Vandana (1998), ukandamizaji wa makundi waliotengwa na ukandamizaji wa mazingira asilia unahusiana. Mfumodume unaohusishwa na sifa za jinsia ya kiume zinaonekana kuwa na thamani zaidi na zimechangia uharibifu wa mazingira (ardhi na wanyama) pamoja na utenguaji wa vikundi mbalimbali vya watu kama vile wanawake, watoto, na watu wenye rangi tofauti. Mfumo wa ubepari pia unaendeleza unyanyasaji kwa vile mfumo huu unasisitiza uzalishaji mali kwa njia zozote bila kujali au kuhusisha jinsia ya kike pamoja na mazingira. Kanuni hii iliufaa utafiti huu katika kubainisha lugha inayotumiwa na jinsia ya kiume wakati wanapotekeleza ukandamizaji wao kwa jinsia ya kike na mazingira yao. Vilevile, tuliweza kuelewa mwitikio wa jinsia ya kike kupitia kwa lugha inayotumiwa na jinsia hii aidha kwa kukubali ukandamizaji na uharibifu wa mazingira au iwapo watakataa ukandamizaji huu pamoja na uharibifu huu wa mazingira.

Vivyo hivyo, mhimili huu uliusaidia utafiti huu kubaini udhihirishaji wa mtazamo wa kijinsia kuhusu wahusika wa jinsia tofauti kwa kuzingatia namna wanavyotumia lugha, kwani jinsia moja huenda ikasheheni mtazamo hasi kuhusu jinsia moja na mtazamo chanya kuhusu jinsia nyingine hasa kwa kuzingatia namna jinsia hizi mbili zinavyotumia lugha ili kuelezea hali mbalimbali zinazowakumba katika mazingira wanamoishi.

Pili, lazima tuubadilishe utamaduni wa kutawaliwa na maadili ya kujali. Merchant (2005) anasema kuwa kimsingi Ekofeministi inahusu maadili ya kujali na maadili yanayoruhusu maamuzi kufanywa kwa usawa. Maadili ya kujali yanamaanisha kuwa, mazingira yanapoharibiwa hata sisi (jinsia mbalimbali) tunaharibiwa. Uharibifu huu unazuka kutokana na mifumodume unaoshikilia kuwa, anayemiliki nguvu za uongozi ana haki ya kutawala, kudhibiti na kutumia kila kitu bila kujali watawaliwa. Kipengele hiki kilimsaidia mtafiti kuweka wazi vipengele vya ekolojia vinavyoathiriwa zaidi kwa kupitia matendo ya jinsia moja au iwapo jinsia zote zinaathiri kwa namna sawa na vipengele vya ekolojia.

**MAPITIO YA MAANDISHI**

**Changamoto za Kimazingira**

Kulingana na makala uliyoandikwa na Mugwe (2018), wito ulitolewa kuhusu athari za matumizi mabaya ya ardhi. Kwa mujibu wa makala hayo, kulikuwa na umuhimu wa kuwajengea uwezo watunga sera hasa makatibu wakuu na wabunge kuhusu athari za matumizi mabaya ya ardhi katika maeneo ya vyanzo vya maji, mito na kandokando ya bahari ili kuwepo na uelewa wa pamoja wa athari hizo na njia za kupambana nazo kwa ubora na kwa manufaa ya nchi na vizazi vitakavyokuja halafu.

Kwa mujibu wa rekodi na takwimu za World vision International (2021), ambalo ni shirika la dunia linalojivunia historia ndefu ya kuchunguza vyanzo mbalimbali vya mabadiliko ya hali ya anga na hata kupendekeza suluhisho faafu kwa majanga anuai ya kimazingira hasa kwa kuweka umakinifu kwa watoto na jamii zilizobaguliwa, mabadiliko ya hali ya anga huathiri kila mmoja huku wavulana na wasichana watokao kwa jamii zilizobaguliwa wakiathirika zaidi kutokana na ukosefu wa rasilmali msingi ya kushughulikia mahitaji yao ya kila siku. Ripoti hii hushikilia kuwa takriban watoto bilioni moja huishi katika nchi ambazo zinapata athari kali za mabadiliko ya hali ya anga. Aidha ripoti inaeleza kuwa uzalishaji wa vyakula umepungua kwa kiwango kubwa sana kwa sababu sehemu kubwa ya ardhi imebaki tabambarare kutokana na shughuli za kibinafsi za watu kama vile ukataji wa miti asilia. Hivyo basi, changamoto nyingi za siku hizi kama vile vita, magonjwa, maafa na ukosefu wa vyakula zimesababishwa na mabadiliko ya hali ya anga hali ambayo inaendelea kuwa mbaya zaidi.

**Suluhisho kwa Changamoto za Kimazingira**

Kwa mujibu wa Garrand (2007), changamoto za kimazingira zinazoonekana kimsingi ni za kisayansi na mijadala mingi kuhusu ongezeko la joto

huhusishwa zaidi na wanaangahewa kuliko watunzi wa mashairi na wahakiki wa fasihi. Kutokana na maoni yake Garrand, maswala ya kimazingira yanaweza kuwasilishwa kwa jamii kupitia fasihi kwani ndiyo taaluma inayoingiliana pakubwa na utamaduni wa jamii na hivyo basi hufikia kila mmoja katika jamii Aidha, kulingana na Kashaigili et al. (2005), alieleza kuwa changamoto nyingi za kimazingira zinazoonekana zinachangiwa na ni matokeo ya shughuli za kibinadamu zinazogusa sekta mbalimbali na hivyo basi utatuzi wa changamoto hizo unahitaji jitihada za pamoja za kila mdau kwenye sekta hizo. Isitoshe, wataalamu mbalimbali wajifunze kupanga mikakati ya pamoja na kukabiliana na majanga ya kimazingira. Aidha ni muhimu kuwasambaza wataalamu mbalimbali kwenye nchi tofauti ili kila taifa lipate uelewa wa pamoja wa kupambana na majanga ya kimazingira.

Kongamano la umoja wa kitaifa kuhusu mazingira na maendeleo (UNCED), tarehe 14, mwezi wa Juni, 1992, lililofanyika Rio de Janeiro, almaarufu Agenda 21, kwa lengo la kusitisha na kupunguza athari zinazoletwa na kudorora kwa mazingira ili kuleta na kuendeleza maendeleo ambayo hayana athari kwenye mazingira katika mataifa yote. Kongamano hili lilichochewa na kuwepo kwa sheria zinazosababisha kuendelea kwa uzorotaji wa mfumo wa kiekolojia na hivyo basi kuangamiza uhai wa binadamu. Kongamano hili vilevile lilipendekeza kwamba juhudi za utunzaji wa mazingira sharti zitekelezwe na watu kutoka nyanja mbalimbali wakiwemo watunzi wa kazi za fasihi na hata wasomi ili waweze kuwafikia kila mmoja katika jamii.

Kwa mujibu wa kongamano hili, ni muhimu vilevile kuangazia vipengele vya ekolojia ambavyo aghalabu huathirika na matendo ya binadamu na namna jinsia mbalimbali wanavyoweka juhudi ili wapate suluhisho la kudumu kwa matatizo ya kiekolojia yanayowakumba.

**MATOKEO YA UTAFITI**

Kulingana na kamusi ya Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (2014), changamoto ni matatizo ambayo yanaweza kukwamiza maendeleo ya kitu au jambo fulani. Katika riwaya ya Nakuruto, changamoto zilizotambulika ni kama: ukame, unyanyasaji wa kijinsia, unyanyasaji wa wafanyikazi, uchafuzi wa mazingira, uharibifu wa vipengele vya ekolojia kupitia matendo ya kibinafsi ya binadamu, ukosefu wa uwajibikaji wa wanajamii kuhusu utunzaji wa vipengele vya ekolojia na ukosefu wa maarifa kuhusu umuhimu wa viambajengo vya ekolojia. Aidha, utafiti ulibainisha suluhisho kwa baadhi ya changamoto za kiekolojia. Katika ukurasa wa tano, tatizo la kimazingira lilijitokeza kama lifuatalo:

> *Ardhi hii kame haikuwa na mti au mmea wowote. Isitoshe, hakukuwa na dalili ya uhai. Ilikuwa imepasukapasuka kutokana na hari iliyokuwa katika sehemu hii ya dunia…Alihisi tu mchanga wenye joto jingi ukimchapa maungoni na kuufunika uso wake kwa vumbi la hudhurungi. Aidha, viumbe vya jangwani waliokuwa wakipeperushwa na upepo mkali walimchapa maungo. Hakuelewa ikiwa viumbe hao walikuwa hai au ni mabaki tu yale aliyoona mapongoni* (Momanyi, 2009, pp. 4-5).

Ukame ni tatizo kubwa la kiekolojia hasa unapokithiri kiasi cha kukosekana kwa mti au mmea wowote, na hakukuwa na dalili yoyote ya uhai. Kiwango hiki cha changamoto huathiri vikali binadamu kwani wanalazimishwa kuhamia kwingine. Hali hii inapotokea, basi vikundi vilivyotengwa, watoto na yeyote asiye na uwezo wa kumudu hali huathirika vikali.

Aidha katika ukurasa wa nane, ukosefu wa utangamano ulidhihirishwa huku wanyama wa pori pamoja na wanyama mifugo wakipigania na kung'anga'ania raslimali chache zilizomo ili waweze kukidhi mahitaji yao ya kila siku.

> *Sasa alitambua kuwa alikuwa katika eneo la uadui ulioshamiri miongoni mwa watu hao. Hakuona simba akilisha*

> *na kundi la mbuzi au swara kama alivyoona huko nyuma. Hapa mipaka ya viumbe hawa ilibainika wazi* (Momanyi, 2009, p. 8).

Uhasama miongoni mwa watu aghalabu husababishwa na changamoto za kimazingira ambazo zinachangia kuwepo kwa uhaba wa chakula na vipengele muhimu vinavyosaidia binadamu na wanyama kujimudu kimaisha. Hali hii huchangia utengano na uadui wakati raslimali zinang'ang'aniwa.

Katika ukurasa wa ishirini, mojawapo ya suluhisho kwa changamoto za kiekolojia ni kama ifuatayo:

> *Lo! Hadithi hiyo imenivutia mno. Bila shaka nyanya huyo alikuwa mwenye busara sana. Nitahifadhi akilini ili nami nimsimulie mwanangu Maridhia…alizihifadhi hadithi hizo moyoni mwake, akamshukuru ajuza. …Baada ya maombi hayo, Nakuruto alimtaka Nashelangai amweleze mumewe yale aliyotaka kumwambia ili waweze kuepuka janga lililokuwa mbele yao…Nisikilize kwa makini mjukuu wangu kwani mkizingatia nitakayowaambia, basi mtaepuka hatari iliyo mbele yenu* (Momanyi, 2009, pp. 20-21).

Wanajamii wanafaa kuhifadhi moyoni mwao matendo ya kijadi zilizotumiwa hapo awali kutatua migogoro ya kiekolojia na hata kuzipitisha amana hizo kwa kizazi cha baadaye ili kuepukana na majanga yanayosababishwa na changamoto za ekolojia. Aidha, wanajamii wanafaa kuzingatia masharti na maagizo yote wanayopewa kuhusu nanma ya kuleta mabadiliko chanya katika ekolojia.

Isitoshe, katika ukurasa wa thelathini na mbili, uchimbaji wa mitaro ilichangia kukauka kwa ziwa kitendo ambacho kilitishia kukatiza maisha na shughuli endelevu za jamii nzima bila huruma. Waendelezi wa shughuli hizi zilizosababisha majanga ya kiekolojia, hawakujua athari za matendo yao kwa jamii na maisha yao ya halafu.

> *Mitaro mingi mnayochimba mahali hapa mtakuja kukausha Ipe Ludao, Nakuruto alitamka kwa sauti kali iliyomshtua Ludao…chanzo cha mwendelezo wa uhai wenu ni Ipe, nanyi mko mbioni kuukatiza…Kando ya ziwa, umati wa wanawake na watoto ulikuwa ukifua nguo. Maji taka yalikuwa yakimiminiwa ziwani mfululizo, povu la sabani lililomwangwa mahali pale kwa miaka mingi tayari lilikuwa limeathiri mazingira ya ziwa. Miti ilikuwa imeanza kupiga manjano kwa sababu ya magadi mengi ya sabuni. Chini kidogo, wanawake wengine walikuwa wakiteka maji huku wakioga* (Momanyi, 2009, pp. 32-33).

Kulingana na maelezo haya, njia mbalimbali zinaibuliwa za kuiwezesha jamii kupata tiba kwa baadhi ya majanga ya kiekolojia. Jamii inahamasishwa kuenzi na kutumia vizuri zawadi walizotunikiwa na Mwenyezi Mungu na kupasafisha mahali panapositiri uhai wa jamii ili maisha ya jamii yasiwe kwenye hatari.

Isitoshe, katika ukurasa wa 35, Nakuruto anatoa tahadhari kwa wanaochafua ziwa,

> *Naomba kutoa tahadhari kwa uchafuzi wa ziwa unaoendelea hapa. Maji taka mnamwaga humo ndani. Nyie wenyewe mnaoga humo ilhali wengine pale chini wanateka maji wakinywa. Wakulima wanazidi kuchimba mitaro mikubwa ya kupitishia maji ya kupitishia maji ya ziwa mashambani mwao. Gugumaji linalootа pale ni tisho kwa uhai wenu na kizazi kijacho. Mfahamu kuwa, ziwa hili husitiriwa na mto mmoja tu* (Momanyi, 2009, p. 35).

Kutokana na maelezo haya, majanga ya kimazingira huathiri zaidi watoto kwa kukosekana kwa lishe ziwa linapokauka. Utamaduni wa kutawaliwa na imani hasi umebadilishwa na maadili ya kujali. Changamoto ya kimazingira yaliyosababishwa na imani hasi ya wanajamii inasuluhishwa wakati wanawake na wanaume wanapokubali makosa yao baada ya kuhamasishwa na Nakuruto, hadi wakakubali

kukomesha uchafuzi wa mazingira. Wanakijiji hivyo basi wanafaa kuweka mikakati ya kutunza ziwa. Aidha, wanakijiji wanafaa kukomesha uchafuzi wa ziwa huku wakulima wakihamasishwa wakomeshe uchimbaji wa mitaro mikubwa inayosababisha kukauka kwa ziwa. Katika ukurasa wa thelathini na saba, majanga ya kimazingira zinazidishwa na ubinafsi unaoendelezwa na matajiri ambao hawajali athari za matendo yao kwa mazingira na maisha ya wanajamii kijumla.

> *Zamani Walatimbi walimiliki maji ya mto huu ambao walizawidiwa na maumbile. Uhai wao ulitegemea mto huu. Lakini sasa uhai wa watu unadhibitiwa na bwenyenye anayewatumikisha bila huruma. Naam, uhai wao unatishwa na nguvu za mamlaka kutoka nje ya kijiji* (Momanyi, 2009, p. 37).

Wanaofanya biashara hawajali athari za matendo yao kwa wanajamii na mazingira kijumla. Wanadhibiti maisha ya wanajamii kwa matendo yao ya kibinafsi ilmuradi wanapata faida hata kama kwa damu na maisha ya wanajamii. Tiba kwa janga hili ni kwamba wanajamii wanafaa kuungana na kukomesha ubinafsi unaoendelezwa na bwenyenye. Isitoshe, biashara yoyote ile inafaa kuyapa kipau mbele maslahi, matarajio na maisha ya binadamu.

> *Aliutazama mto ule jinsi ulivyobinafsishwa na mtu mmoja huku kijiji kizima kikisota bila maji. Bw. Brook aliyamiliki maji yale akawanyima wanakijiji kuyateka kwa matumizi yao ya nyumbani. Iliwabidi Walatimbi kuyanunua kutoka katika mifereji aliyoimarisha bwenyenye huyo…* (Momanyi, 2009, p. 38).

Kuna changamoto kuwa wanakijiji wanahangaika kwa kukosa maji ambayo hapo awali walikuwa wamezawadiwa na maumbile. Uhai wao ulitegemea mto huo. Lakini sasa uhai wao unadhibitiwa na bwenyenye ambaye anawatumikisha bila huruma. Wanaekofeministi wanashikilia kuwa ukandamizaji wa aina zozote zinahusiana na hazikubaliki. Wana Walatimbi hatimaye walikataa kuukubali ukandamizaji baada ya kuzinduliwa na Nakuruto, wakakataa ukandamizaji wa bwenyenye kwa kusanyika na kuweka mipango hatua baada ya hatua kwa kulivamia lile kasri la Bw. Brook, hadi wakarejesha maji yao.

Baadhi ya wahojiwa walikubaliana na kauli kuwa lugha ya kijinsia ina nafasi kubwa katika kusuluhisha matatizo ya ekolojia. Mhojiwa mmoja alisimulia kisa cha Profesa Wangari Maathai katika kutatua changamoto za kimazingira. Alisema kuwa wakati ulifika alipotishia serikali ya Rais Moi kuwa angejisasambura au kuvua uchi ili kuokoa bustani la *Uhuru Park* dhidi ya unyakuzi na wawekezaji wa kibinafsi. Kutokana na swala hili, ilibainika kuwa lugha ya wanawake pia inaweza ikawa ya vitisho hususan kwa kutumia sehemu nyeti za miili ili kuzuia mabaya kutendeka katika mazingira na pia katika kupigania haki.

Katika ukurasa 56-57, mawazo ya Nakuruto yanachimuzwa pale ambapo tunaelezwa kuwa:

> *Miti yote ikachomwa makaa. Mvua zikahama kabisa. Ukame ndio ukawa maambilio yetu. Zitoke wapi miti imekatwa yote? Kuna changamoto kubwa kuwa hamna mvua kabisa kwa sababu ya ukosefu wa miti ambayo tayari imekatwa* (Momanyi, 2009, p. 56).

Changamoto kubwa ya kimazingira katika kizazi hiki ni ukataji wa mti kwa manufaa ya kibinafsi bila kujali kuipanda miti mingine. Jinsia mbalimbali huchoma makaa ili iweze kujimudu kiuchumi. Hali hii husababisha janga kubwa zaidi hasa mvua inapokosekana na jamii kubaki bila chakula. Chakula kinapokosekana, njaa hushamiri na kutawala, magonjwa na vifo havikosekani katu! Hivyo basi, wanajamii wanafaa kubuni namna mbadala ya kuwawezesha kujikimu kimaisha. Wanaotumia makaa vilevile wafaa kutumia namna tofauti ya kupata umeme wa kupikia kama vile gesi na hata stima. Isitoshe, miti inapokatwa, ni vyema na muhimu miti mingine zaidi kupandwa.

Katika ukurasa wa hamsini na tisa, majanga mengine ya kimazingira ni kama yafuatayo:

> *Machimbo hayo yamepoteza watoto wetu wengi mno mama. Wengine wameangukiwa na majabali humo*

> *wakazikwa wakiwa hai. Wengine wamezirai humo kutokana na ukosefu wa hewa ya kutosha na wengine mvua zikanyesha, mashimo yakajaa maji na kuwazamisha kabisa. Isitoshe mjukuu wangu, kiwanda hicho kimekuwa tisho kwa uhai wa wanakijiji. Hewa ya sumu itokayo kiwandani imesababisha vifo vya watu, wakiwemo watoto. Wanaoathirika huanza kukohoa kisha hupata shida ya kupumua. Baadaye huzirai na kufariki…* (Momanyi, 2009, p. 60).

Swala la matajiri waliosaki inda na ubinafsi limekuwa sugu katika mambo yanayohusu ekolojia na maisha ya binadamu. Wengi wameathirika na hata kupoteza maisha, lakini hatua ya kisheria bado haichukuliwi. Ni bayana kulingana na hitaji la sera za kibinadamu kwamba viwanda havifai kuwekwa karibu na mastakimu ya binadamu hasa vinapofuka hewa ya sumu. Changamoto hili halijapata suluhisho la kudumu kwa sababu ya ubinafsi, ufisadi na kutojali maisha ya jamii hasa wale walio na pato la chini.

Katika ukurasa wa mia moja na arobanne, mojawapo wa vyanzo vya majanga ya kimazingira ni kule watoto kukosa waelekezi na elimu kuhusu umuhimu wa kuhifadhi mazingira.

> *Watoto walikuwa kama kondoo waliokosa wachungaji. Walezi waliacha majukumu ya kuwalea wakaingia kwenye mbio ya kusaka harufu ya nta. Aidha, pale alipokuwa, alishuhudia pia kusambaritika kwa taasisi za vijiji. Mashamba ya vijijini yaliacha kulimwa, watu wakakimbilia mashamba makubwa makubwa yenye kuzalisha mazao ya kusafirishwa nje ya vijiji. Konde za watu zikamea magugu kwa kukosa huduma. Hata wale waliokuwa wakilima ili kukidhi mahitaji yao, walitenga ardhi kubwa ya vikataa vyao kukuza mazao yaliyoweza kutega harufu ya nta. Taratibu za masomo kwenye taasisi za elimu zikabadilishwa…Nidhamu ikazoroteka miongoni mwa vijani kwani mafunzo ya kimaadili yaliondolewa katika taratibu za masomo. Viwanda vikaanza kuzalisha bidhaa zilizolenga kuinasa harufu hiyo bila kujali maslahi ya waliozalisha. Nakuruto akaona afya za wanavijiji wengi zikizoroteka…* (Momanyi, 2009, p. 140).

Kupata suluhu kwa majanga ya kiekolojia kunataka uamuzi wa kibinafsi, huku kila mmoja katika jamii akijituma na kubadilika ili jamii ipate suluhu ya kudumu kwa changamoto zinazoikabali jamii na kutishia na hata kuumaliza uhai wao. Isitoshe, kila jamii inafaa ijielewe vyema kabla haijapapia mageni bila kuelewa athari yake ya halafu kwa maisha ya wanajamii kijumla. Dai hili limeungwa mkono na wanakikundi lengwa pamoja na watoa taarifa katika usaili kwamba, ili maendeleo ya kudumu yapatikane kuhusu ekolojia, basi kila mmoja lazima ajibidiishe kujenga ngazi ya mabadiliko kwa manufaa yao wenyewe na hata kwa vizazi vingi vijavyo.

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

**Hitimisho**: Utafiti ulibaini kuwa jinsia ya kike imetengwa katika kutatua changamoto za kiekolojia katika riwaya ya *Nakuruto.* Utafiti ulionyesha kuwa jinsia zote zina nafasi kubwa katika kutatua migogoro katika mazingira na kuurejesha uhai katika ekolojia.

Changamoto: ni kama zifuatazo; ukame, uchafuzi wa mazingira, uharibifu wa vipengele vya ekolojia, njaa, unyanyasaji wa kijinsia, uchafuzi wa hewa hasa kwa moshi kutoka kwa viwanda, matendo hasi ya kibinafsi kutoka mabwenyenye, taasubi ya kiume na ukosefu wa elimu kuhusu umuhimu wa kutunza mazingira.

Suluhisho: ni kama zifuatazo; kuhifadhi moyoni matendo ya kijadi yaliyotumiwa kutunza mazingira na kuyapitisha kwa vizazi vijavyo, kuzingatia masharti na maagizo kuhusu uhifadhi wa ekolojia, kuwazuia waharibifu wa vipengele vya ekolojia, jamii kuhamasishwa kuhusu majanga ya kiekolojia na namna ya kuepuka majanga hayo, kupasafisha maeneo yanayositiri uhai wa jamii, wanajamii kuungana na kukomesha matendo hasi ya kibinafsi yanayoharibu mazingira.

**Mapendekezo**: Kutokana na athari za lugha ya kijinsia katika kusuluhisha majanga ya kimazingira, utafiti mbadala unafaa uangazie nafasi ya jinsia ya kiume katika kusuluhisha matatizo ya kiekolojia. Kwa vile utafiti huu uliangazia uhakiki wa jinsia kuhusu fasihi ekolojia katika riwaya ya *Nakuruto*, utafiti huu unapendekeza kuwa tamthilia na hadithi fupi, hususan

ya kijinsia pia yapate kufanyiwa utafiti. Aidha jinsia zote zipate nafasi sawa katika utunzaji wa mazingira. Jamii nzima inapaswa kuhamasishwa kuhusu majanga ya kiekolojia na namna ya kuepuka majanga hayo, kupasafisha maeneo yanayositiri uhai wa jamii, wanajamii kuungana na kukomesha matendo hasi ya kibinafsi yanayoharibu mazingira.

**MAREJELEO**


Garrand, G. (2007). *Ecocriticism and education for sustainable pedagogy*. Duke University Press.

Glotfelty, C., & Fromm, H. (Eds.). (1996). *The ecocriticism reader: Landmarks in literary ecology*. University of Georgia Press.

Intergovernmental Panel on Climate Change. (2014). *Climate change 2014: Mitigation of climate change: Contribution of Working Group III to the Fifth Assessment Report of the Intergovernmental Panel on Climate Change*. Cambridge University Press.

Kashaigili, J. J., Kadigi, R. M. J., Lankford, B. A., Mahoo, H. F., & Mashauri, D. A. (2005). Environmental flows allocation in river basins: Exploring allocation challenges and options in the Great Ruaha River catchment in Tanzania. *Physics and Chemistry of the Earth, Parts A/B/C, 30*(11–16), 689–697. https://doi.org/10.1016/j.pce.2005.08.009

Krebs, C. (1978). *The experimental analysis of distribution and abundance*. Harper Limited.

Libre, V. (2022, November). *Texts global*. https://query.libretexts.org/Kiswahili

Matti, G. (2003). *Mwongozo wa Kitumbua kimeingia mchanga*. Africanwide Network.

Mbogo, E. (2002). *Bustani ya Edeni*. MPB Enterprises.

Mberia, K. (2001). *Bara jingine*. Marimba Publishers.

Merchant, C. (2005). *Ecofeminism*. Routledge.

Momanyi, C. (2009). *Nakuruto*. Sasa Sema Publications.

Mugwe, J. (2018). *Athari za mtagusano kati ya jamii na ekolojia katika ushairi wa Kithaka wa Mberia: Bara jingine na Rangi ya Anga* [Master's thesis, University of Nairobi].

Odum, E. (1971). *Fundamentals of ecology*. Sage Publishers.

Rannard, G., & Stallard, E. (2022, November 20). *COP27: What have global leaders done on climate change in 2022?* BBC News.

Stoddart, M. C. J., & Tindall, D. B. (2011). Ecofeminism, hegemonic masculinity, and environmental movement participation in British Columbia, Canada, 1998–2007: "Women always clean up the mess." *Sociological Spectrum, 31*(3), 342–368. https://doi.org/10.1080/02732173.2011.557065

Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. (2014). *Kamusi ya Kiswahili sanifu*. Oxford University Press.

Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. (2019). *Kamusi ya Kiswahili sanifu*. Oxford University Press.

Vandana, S. (1988). *Staying alive: Women, ecology and development*. Sage Publishers.

Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha fasihi: Simulizi na andishi*. Focus Publications.

World Vision International. (2021, November 8). *Climate change, hunger and children's futures*. World Vision International.